
# THE SACRED NAME BROADCASTER

## Mtangazaji wa Jina Takatifu



11/2024

*a publication of* ***Assemblies of Yahweh***

# THE SACRED NAME BROADCASTER

An ***Assemblies of Yahweh*** *publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***November 2024***
***Volume LVI, Number 7***


# YALIYOMO











***1 Kr-smasi: Utaitunza Mwaka Huu?***
*Kila desturi ambayo tunatunza Lazima ichunguzwe na Sheria ya Yahweh. Utafuata nini Maandishi yanafunza kuhusu X-masi?*

***9 Kr-smasi kama Inavyofunza Biblia***
*Umewahi kustaajabu kwa nini Wakr-sto wanatunza Kr-smasi wakati haijatajwa kamwe katika Biblia? Kwa nini dini ya kidunia imetakasa sikukuu ya upagani?*

***14 Sheria Ya Yahweh: Amri ya Nane Usiibe***
*Wizi unaweza kufidiwa kwa urejeshaji, kulingana kwa sheria ya Yahweh, Kutoka 22:2.*


***19 Tena Majani Yanaanguka***
*Shairi na Mzee Jacob O. Meyer (OBM) inayoakisi mwendo wa kasi wa wakati.*

***21 Mwelekeo wa Kinabii: Nakala ya Sanduku Mpya Yafichuliwa***
*Picha za kuvutia na ripoti. Hekalu litajengwa tena karibuni?*


## Jalada Letu

*Rangi ya kung'aa ya majani yaliyochorwa na ubao wa Yahweh, Muumba wetu, huweka alama mwisho wa msimu mwingine wa upanzi.* ***"Katika ardhi, Yahweh Elohim akachipusha kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa...."*** *(Mwanzo 2:9a).*

*Kama tutaweka imani katika Yahweh, ameahidi kwamba tutakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji ambao utadumu kila wakati wa ukame-bado ukizaa matunda. (Yeremia 17:7-8).*




*Yahshua alitumia mlinganisho wa mti unaozaa matunda mema* ***"Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake kuwa mazuri; au ufanyeni mti kuwa mbaya na matunda yake mabaya, kwa maana kwa matunda yake mti hutambulikana."*** *(Mathayo 12:33). Unazaa matunda mema?*

***"Mwenye haki atastawi kama mtende, atakua kama mwerezi wa Lebanoni. Waliopandwa katika nyumba ya Yahweh, watastawi katika nyua za Elohim wetu. Watazaa matunda hadi wakati wa uzee, watajaa utomvu, watakuwa na ubichi. Watangaze ya kuwa Yahweh ni mwenye adili, mwamba wangu, ndani yake hamna udhalimu."*** *(Zaburi 92:12-15).*

*Kuwa mti wa haki- upandaji wa Yahweh- kwa kuishi maisha yanayomtukuza Yahweh kila siku?* ***"Wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Yahweh, ili atukuzwe."*** *(Isaya 61:3b).*


Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.



© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.


Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:*** *Mzee Jacob O. Meyer*

# Chr-stmas

# Krismasi: Utaitunza Mwaka Huu?

**Na Mzee Jacob O. Meyer**

Watu mara nyingi hufuata mila zilizowekwa na jamii bila kuuliza kwanza wapi mila zilizoheshimiwa za nyakati hizi zilitokea. Wanadhani kwamba ulimwengu kando yao unaonyesha kwa usahihi jinsi watu wanapaswa kuishi. Ni imani yao kwamba, kwani madhehebu mbalimbali ya Ukristo wa kawaida wanatumia Biblia katika mafundisho yao, kwa uaminifu wanafuata njia ya maisha ya kibiblia na desturi na mila wanazoweka.

Walakini, Biblia yako inaonya daima dhidi ya kukubali njia za ulimwengu. Yeremia 10:2 inatushauri tusijifunze njia za mataifa (neno la Kiebrania ni *goyim*, kumaanisha *mataifa ya ulimwengu*). Mstari uliowekwa kati ya matendo ya Kusanyiko la kimitume kwa upande mmoja na mtindo wa maisha wa kidini wa dunia kwa mwingine, unaendeshwa nyumbani kwa uhakika na umati mkubwa wa Maandiko. Kwa sababu tu mamilioni ya watu wanafanya kitu fulani sio ishara wazi kitendo hicho kwa asili kilitolewa kwa Biblia.

Mwenye-nguvu Yahweh alimtoa Ibrahimu Uri wa Wakalidayo, akimweka katika eneo la nchi ya vilima ya Kanani. Mwenye-nguvu Yahweh alimfunza Ibrahimu njia ya Kweli. Maelezo kama hayo ya kimwili yanaweza kuelezewa kiroho kumaanisha kwamba Yahweh alimleta Ibrahimu kutoka kwa mfumo uliozorota wa ulimwengu na kumfunza njia ya kweli kwa maisha ya milele katika mahali palipojitenga, kama sisi, wa Assemblies of Yahweh leo, tu-



## *Kwanini Wakristo wanasherehekea Kr-smasi Desemba 25?*

# *YAHSHUA ALIYE MESSIAH HAKUZALIWA DESEMBA 25.*

navyofunzwa. Israeli, kizazi cha Ibrahimu walitolewa Misri na kukaa miaka 40 nyikani wakijifunza njia ya Yahweh. Paulo anaelezea tukio hili katika Matendo ya Mitume 13:18 kwa kusema, ***"Na kwa muda wa miaka arobaini kama baba anayenyonyesha, akawavumilia katika jangwa."***Yahweh alikusudia Israeli kuacha nyuma njia za jamii hiyo ya dhambi. Yahweh alikusudia Israeli kutoa ushahidi jasiri kwa njia ya maisha ya mbinguni kwa mataifa waliomzunguka. Biblia yako inayo rekodi ya maendeleo na kushindwa kwa watu waliopaswa kuwa mashahidi wa Yahweh.

Kwa miaka kadhaa, ofisini mwa mwandishi, faili ya nakala za gazeti na jarida zinazohusiana na asili ya upagani ya mila zilizoambatanishwa kwa sherehe ya Krismasi imekuwa ikikua. Nikisoma yaliyo kwa faili hii katika matayarisho kwa kuandika muundo huu ilikuwa tena ya kuelimisha sana. Waandishi wengi walioandika nakala hizi za kuelimisha walifahamu kikamilifu na kuelewa asili ya upagani ya desturi na mila zinazotunzwa wakati wa krismasi (vilevile kama sikukuu zingine zinazoadhimishwa na dunia). Hata hivyo, wachache na walio mbali na wenzao ni watu walioamua ambao kweli wanatetea kuondoa mila hizo kutoka kwa matendo yao. Wakati wanajua na kuelewa kweli hizi halisi, bado hawatajiruhusu wenyewe kusahihishwa na ushahidi wa kibiblia na wa kidunia. Watu wengi wa dunia wanaonyesha mtazamo huu mkaidi.

Kweli u mtu mwenye mawazo wazi? Umejitolea maisha yako binafsi kumtumikia pekee yake Aliye Juu Baba wa Mbinguni? Utaongozwa na Neno la Yahweh Aliye Juu? Unairuhusu kwa unyenyekevu Biblia kukusahihisha? Kama unaweza jibu kwa kukubali kwa maswali haya yote, basi tungekuhimiza usome nakala hii kwa uangalifu sana. Angalia kweli hizi wewe mwenyewe, kisha fanya maamuzi yako. Ukweli uliochapishwa hapa unaweza kuthibitishwa katika maktaba iliyo na kazi za marejeleo yaliyonukuliwa. Lakini, kumbuka kweli hizi hazitakufaidi isipokuwa ufanye kitendo juu ya habari kwa kuleta maisha yako binafsi katika maelewano kwa yale inakukataza.

### Kushindana na Upagani

Wakati Kusanyiko la Kimitume lilikuja kuwepo, washiriki walijitolea kabisa kufanya matayarisho yao kwa Ujio wa Mara ya Pili wa Yahshua aliye Messiah. Kusanyiko la kimitume la kitabu cha Matendo ya Mitume kamwe halikuwa kubwa kiidadi. Lilikuwa kundi ndogo, lakini lilijitolea kabisa kutii ukweli wa neno la Yahweh.

Ndugu wa kusanyiko la mitume walijipata wenyewe katikati mwa serikali yenye nguvu sana- Ufalme wa Kirumi. Dini ya ufalme huu mkubwa ilikuwa na msingi wa awali juu ya ule wa Ugiriki wa kale. Katika Pantheoni- jengo kubwa lililo mji wa Rumi- kila dini kubwa iliwakilishwa, na picha ya kila mwenye-nguvu ilikuwa imewekwa. Kwanza miongoni mwa wenye-nguvu hawa wa upagani alikuwa Jupita, wa Kilatini wa kulingana na kiwakilishi cha mwenye-nguvu wa kale wa Ugiriki- Zeus. Dini ya Jupita na Zeus (baba ya wenye-nguvu) ilikuwa na nguvu hivyo na iliwekwa juu ya akili za watu wa kale kwamba, dhahiri, baadhi ya mawazo hayo ya kidini ya upagani hatimaye yalibebwa kwenye Kusanyiko la kimessiah na watu waliokuwa wameanza kufuata Imani ya kibiblia.

Desemba 25 ilikuwa siku takatifu ya kalenda kwa uabudu wa Zeus na wenye-nguvu wengine wa upagani. Baadhi ya waandishi hata wanadai kwamba Zeus alizaliwa Desemba 25. Siku hii inaitwa *winter solstice* wakati jua linaonekana kusimama tuli mbinguni kama linaondoka kuelekea kusini na, siku kadhaa baadaye, linarejea safari yake inayofuata kaskazini, kuashiria majira ya joto nyingine.

Basi tutambue nini tunapata katika 1 Makabayo 1:52-64.

*"Wengi wakajiunga nao, yaani wao waliokuwa wameasi sheria; wakafanya maovu katika nchi hata Waisraeli walilazimika wajifiche katika makimbilio ya siri huko na huko.*

*"Siku ya kumi na tano ya*

*Kislevu, mwaka wa mia arobaini na tano, waliweka chukizo la uharibifu juu ya madhabahu, na katika miji ya Uyahudi kila upande walijenga madhabahu, wakavukizia uvumba milangoni pa nyumba na njiani. Na vitabu vya sheria walivyovipata walivirarua vipande vipande wakaviteketeza. Mtu yeyote aliyepatikana na kitabu, au aliyeonekana anaifuata sheria, alihukumiwa kufa kama alivyoamuru mfalme. Hivyo ndivyo walivyowatenda Waisraeli kwa jeuri, wale walioonekana mwezi kwa mwezi katika miji. Na siku ya ishirini na tano ya mwezi walitoa dhabihu katika madhabahu iliyowekwa juu ya madhabahu. Nao wanawake waliowatahiri watoto wao waliwaua kama ilivyoamriwa, wakitungika wana wao shingoni mwao; wakawaua wote wa nyumbani mwao, na wale waliowatahiri watoto.*

*"Hata hivyo wengi katika Israeli walikaza nia zao kwa uthabiti wasile vitu vilivyo najisi. Waliona afadhali kufa kuliko kutiwa unajisi kwa vyakula au kulivunja agano takatifu. Wakafa.Na Israeli akateseka sana*." **The Complete Bible, An American Tradition**.

Kwa nini Wakr-sto wanasherehekea Kr-smasi, Desemba 25?YAHSHUA ALIYE MESSIAH HAKUZALIWA DESEMBA 25.Nakala yetu iliyochapishwa juu ya somo hili itathibitisha kauli hii ya ukweli kwako ikiwa unayo akili wazi.Maandishi yanaonyesha kwamba Yahshua aliye Messiah alizaliwa siku ya kwanza ya Sikukuu ya vibanda katika vuli ya mwaka. Hili linaweza kuthibitishwa kutoka Luka mlango wa 1. Pia Yohana 1:14 inapaswa kuzingatiwa.***"Naye Neno alifanyika mwili, akafanya vibanda nasi (nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba), amejaa neema na kweli."***

Neno *Kr-smasi* kweli linamaanisha *misa ya kr-sto*, misa inayofanywa katika sherehe ya kuzaliwa kwake. Unaweza kuthibitisha hili kutoka kwa kamusi yoyote nzuri. Kama Yahshua aliye Messiah hakuzaliwa wakati huu wa mwaka, kwa nini utunze Siku Yake ya kuzaliwa?

Zaidi, vipi muumini Mprotestani anaweza kutunza siku yoyote iliyotolewa kufanya misa, adhimisho la Ukatoliki wa Kirumi? Vipi Mprotestanti anaweza lalamika tena anapojiunga katika ibada na wale anaolalamika dhahiri dhidi yao? Umechanganyikiwa sasa? Ulijua kwamba mkanganyiko ni maana ya "Babeli"?

Kwani ni viwakilishi vya uabudu sanamu vinavyowakilisha ibada ya jua, wengi wa wenye-nguvu wa upagani walizaliwa karibu msimu wa baridi ambao uliwekwa kizamani Desemba 25. Siku ya kuzaliwa ya Mithra iliangukia Desemba 25. Mithra aliashiria jua, kama walivyo wenye-nguvu wengine wa mataifa kama Osiris, Hercules, na Bacchus, waliosemekana kuzaliwa siku hiyo. Ya kuvutia, mwokozi wa upagani wa Uchina, Zas, alizaliwa Desemba 25. (Umegundua mfanano wa karibu kwa neno *Zeus* la Kigiriki?) kuongezea mwenye-nguvu wa kimisri Horus, mwenye-nguvu wa Kihindi Vishnu, na wa Ashuri Tammuz walikuwa na siku yao ya kuzaliwa Desemba 25, kama alivyo Mwenye-nguvu Dionysus wa Ugiriki, aliyekuwa utambulisho wa Zeus.




**Picha ndogo ya Bas-inayoonyesha Mithras akimtazama Sol Invictus huku akimchinja fahali. Sol na Luna wanaonekana juu ya eneo.**



Lazima tutaje kuwa ibada ya jua inawakilisha ufunguo wa kuelewa kwa nini Kr-smasi inaadhimishwa Desemba 25. Mzunguko wa msimu wa dunia kuzunguka jua ulikuwa wenye wasiwasi mkubwa kwa watu wa kale wakulima. Katika usiku kati ya Desemba 24 na 25, jua lilitambuliwa kuwa limepita sehemu ya mbali kabisa kutoka dunia na lilikuwa linaanza safari yake mpya kurudi kutoka kusini hadi kaskazini. Kwani jua hutoa mwanga wa ulimwengu na kutoa joto kwa dunia na ukuaji wa mimea, baridi na njaa ingeangamiza bila kuepukika taifa la binadamu ikiwa jua halikurejea kutoka kusini. Kwa sababu hiyo, katika maeneo ya kaskazini ambapo ustaarabu mwingi wa mapema ulitokea, furaha kubwa ilitokea wakati watu walihisi kwamba jua limesimama katika kutoka kwake duniani na sasa lilikuwa linarudi. Hivi ndivyo desturi hiyo ya mithiolojia kama Kr-smasi ilianzia.

Dini za mataifa ya kale waliita jua Mwokozi wao. Kwani mwokozi wa jua alikuja, au kurudi, kuokoa ulimwengu kutoka kuteseka majira kali ya baridi, ilimaanisha kwamba maisha mapya na tumaini ilitolewa kwa watu wa dunia. Kwa hivyo, waweza kutambua jinsi dhana hizi za upagani zimebakia katika baadhi ya nyimbo za Kr-smasi. Nyimbo ambazo kweli hazionyeshi ujumbe wa kweli wa kibiblia zinaimbwa katika kusifu kuzaliwa kwa mwokozi wao.

Uhusiano wazi kati ya upagani wa kale wa ibada ya jua na sherehe ya kisasa ya Kr-smasi unaweza kwa urahisi kutambuliwa

### Desturi za Kirumi

Katika Rumi ya kale, wakati wa Saturnalia na Brumalia uliwekwa kwa tarehe katika Desemba katikati. Sikukuu hizi zilijulikana kama*Paganalia*. Jina *Saturn* linamaanisha *tele*. Desturi tofauti za saturnalia ni karibu kwa zile za Kr-smasi kama inavyosherehekewa leo.

Hapa ni uhakiki wa baadhi ya mila hizo za Kirumi. Thibitisha madai yetu kutoka kwa ensaiklopedia nzuri. Sherehe kubwa zilifanyika kote katika siku ya Saturnalia. Watumwa walipewa uhuru kwa siku na mara nyingi walihudumiwa na wakuu wao kwenye sherehe. Kulikuwa na kusimamishwa kwa jumla kwa shughuli zote za umma. Korti na shule zilipumzika; shughuli zote za kibishara na kijeshi ziliahirishwa. Maarufu zaidi miongoni mwa chakula za sherehe iliyopakuliwa ilikuwa kichwa cha nguruwe na tufaha au chungwa mdomoni mwake, pudding ya plamu, mikate ya kusaga, pipi zilizopambwa, vidakuzi kwa kitindamlo, wanasesere walitolewa sana kama zawadi. Baadhi ya wanahistoria wanaunganisha wanasesere hawa kwa sadaka za binadamu kwani sadaka za binadamu zilitolewa *Saturn* wakati mmoja. Neno *Brumalia* linamaanisha *msimu wa baridi*. Neno *solstice* linakuja kutoka kwa mchanganyiko wa maneno kumaanisha jua(neno la kilatini *sol*) likisimama tuli.

Kuongezea, gwaride na *mummeries*, kama vile mtu atapata wakati wetu katika Pasadena Rose Parade na Philadelphia Mummers Parade, zilifanywa katika saturnalia. Tafrija kama hiyo iliunda sehemu muhimu ya maadhimisho yaliyopanuliwa ya

Saturn katika majira ya baridi jinsi tu yafanyavyo leo na sherehe za Kr-smasi/mwaka mpya. Kama mtu yeyote angesafirishwa kwa zama zetu kutoka nyakati hizo za kale, anaweza kuhitimisha kwamba yuko nyumbani haswa katika Maadhimisho ya kisasa ya Krismasi/Mwaka mpya. Kweli, inawezekana kwamba maadhimisho ya siku nane ya leo ya krismasi/ Mwaka mpya yamechukua nafasi ya sherehe ya Yahweh ya kila mwaka inayoitwa Sikukuu ya Vibanda (Walawi 23:33-44).

### Desturi za Norse

Ya kawaida katika baadhi ya nchi za Ulaya haswa Uingereza ni gogo la *yule*. Neno *yule*, kulingana na **Webster's New World Dictionary of the American Language**, Second College Edition, inafafanuliwa kama *jina la kiasili la sherehe ya mataifa katika msimu wa baridi sawa na Jol wa zamani wa Norse*. Kutoka kwa sherehe ya Old Norse linakuja neno *jolly*, linalotumika mara mingi zaidi kwa msimu wa kr-smasi kuelezea tafrija ambayo haiwezi kuungwa mkono kimaandiko.

Ni ya kuvutia kutambua kuwa neno *yule* pia linamaanisha gurudumu katika lugha ya kale ya Norse. Katika Scandinavia sherehe za *yule* ziliheshimu mwenye-nguvu Woden na kuzaliwa tena kwa jua lenye umbo la gurudumu. Kutumia chochote chenye gurudumu wakati wa wiki mbili za kufurahia (kazi iliahirishwa), kama vile gari au gurudumu linalozunguka, ingekuwa tusi kwa jua, ikimaanisha kuwa haikuwa inasonga kaskazini haraka vya kutosha. Kuharakisha kurudi kwa jua, watu wa kale waliunda moto kubwa (moto wa *yule* na magogo). Mitego na nyavu za samaki pia zililetwa ili kwamba hata samaki, ndege, na wanyama wanaweza kupata *yuletides* (wiki mbili, siku kumi na nne, siku 12 za siku za wiki pamoja na Jumapili mbili) wakati wa amani. Katika Wakaldayo wa kale, *yule* ilimaanisha *sherehe ya mtoto*. *Yule* inayo uhusiano tofauti kwa neno la Kisemitiki kwa mtoto au kuzaa- *yeled* na *yalad*.

Kuwasha gogo la yule iliashiria mwanzo wa furaha ya sikukuu. Katika Briteni ilikuwa sherehe ya kidini kwa Druids waliobariki gogo.Mabaki ya moto ya gogo la mwaka uliopita yalitumika kuwasha moto mpya. Moto unaowaka uliashiria nyumbani na usalama. Teutons waliamini kuchoma kwa gogo la *yule* inawakilisha kifo cha jua kuukuu, na mti wa kijani wa kr-smasi ulisimamla kwa kuzaliwa tena kila mwaka kwa mwokozi jua. Warumi waliita kuzaliwa tena kila mwaka *sol invictus*- jua lililoshindwa.

Simulizi ya Santa Claus akiingia kwa bomba la moshi pia lilitolewa kwa Norsemen wa mapema.Hadithi zao zinaambia kuhusu mwenye-nguvu anayeitwa Hertha akionekana kwenye makaa ya mahali pa moto akileta bahati nzuri kwa nyumba. Kwa hivyo, mtu aina ya Santa Claus aliteremka bomba la moshi la watu wa Norse wa kale.

Santa Claus kawaida anaitwa jina *Old Nick*. Unaweza thibitisha kwako kuwa hili lilikuwa moja ya majina ya Shetani kwa kuangalia neno *Nick* katika kamusi yoyote. Shetani amekuwa akijigeuza chini ya majina tofauti kujiletea uabudu kwake.(Hili linaifanya fundisho la Jina Takatifu lenye uzito zaidi.) Neno *Santa*kwa kweli linamaanisha *mtakatifu*, na alitakiwa kuitwa *Saint Nicholas*. Utagundua katika Ufunuo 2:6 na 15 neno *Wanikolai*, limetolewa kutoka kwa neno la Ugiriki *Nike*. Alikuwa mshindi mwenye mabawa ambaye, katika mithiolojia alikuwa mwiinjilisti wa Zeus. Santa Claus anasemekana kuwa ufupisho wa neno *Saint Nicholas* na neno hili basi linaweza wakili-



sha jina linalohusiana na Nike. Santa Claus kwa hivyo alitumwa kutangaza kuja, au kuzaliwa kwa mwaka, kwa mwenye-nguvu wa jua, Zeus.

Baadhi ya imani za jadi ni kwamba hadithi ya sasa ya Santa Claus iliendelezwa kutoka kwa kweli, Mtakatifu Nikolao aliyeishi katika karne ya 14. Alipewa sifa na upagani wa kimiujiza. Kulingana na hadithi moja, alirusha mifuko ya dhahabu kwenye madirisha ya wasichana watatu ambao hawakuwa na mahari, lakini walitaka kuolewa. Baadhi wanaamini kuwa hapo ndipo mila ya kutoa zawadi za kr-smasi ilianzia. Mamajusi utakumbuka, hawakutoa zawadi mmoja kwa mwingine, lakini walizipa kwa Mwokozi, Yahshua aliye Messiah.

Clement Moore, katika 1822, aliandika mtungo, "**The Night Before Christmas**." Mchora katuni Thomas Nast 1863, alimvisha Santa Claus suti nyekundu na kulungu na midolina na kumfanya ateremke bomba la moshi usiku wa krismasi. Walakini, kundi nzima la desturi hii ina msingi juu ya kuwaambia watoto uongo, kwa ujanja kudhoofisha imani yao katika ukweli uliosemwa.

### Ibada ya Mti

Mti wa kr-smasi ni wa upagani kabisa pia. Utaona katoka Yeremia 10:2-4 kifungu cha kimaandiko ambacho kinahusiana kwa ukaribu kwa ibada ya mti. ***"Yahweh asema hivi, Msijifunze njia za mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo. Maana desturi za watu hao ni ubatili, maana mtu mmoja hukata mti mwituni, kazi ya mikono ya fundi na shoka. Huupamba kwa fedha na dhahabu; huukaza kwa misumari na nyundo, usitikisike."*** Ni maelezo gani bora tungeunda kuelezea mti wa siku za kisasa wa Krismasi? Lakini Yahweh alitabiri kwetu zaidi ya miaka 2500 iliyopita.




Katika Marekani, mti wa Krismasi uliletwa kwenye pwani zetu na wahamiaji wa Ujerumani. Mapema kabla ya kupata mila, ibada kwa kutumia mti ilikuwa mila ya kidesturi katika Mashariki ya Kati ya kale. Heshima kwa miti ina tarehe ya nyuma kwa Nimrod, ambaye kifo chake kiliwakilishwa na kukatwa kwa mti.

***Ingeonekana kama mila mingi za Kr-smasi zimetolewa moja kwa moja kwa mpinga-messiah wa kale na mwokozi wa uongo, Nimrodi, na bibi-mama, Semiramis. Ulimwengu leo unaabudu Mwokozi wa uongo na mpinga-messiah chini ya kivuli cha ibada ya jua***

Aescalapius, tabibu au mponyaji, alionyeshwa kama nyoka alijifunga kuzunguka kisiki kilichokufa, ambacho juu yake ilitokea chipukizi mpya kutoka kwa mizizi yake kwa kuzaliwa upya, au kuzaliwa tena kwa mwanawe Nimrodi-Tamuzi. Ibada hii ya sanamu ya Babeli inaendelea kupitishwa kila mwaka katika wakati wa Kr-smasi.

Kushangaza, mamajusi hawakufika kutoa heshima kwa Mwokozi wakati mmoja kama walivyofanya wachungaji, ingawa wanaonyeshwa hivyo katika eneo la kuzaliwa. Wachungaji wakikaa nyanjani karibu Bethlehemu (Luka 2) wangekuwa bila shaka wakitunza wanyama wa sadaka kwa Sikukuu za Vibanda. Walichunga wanyama wao katika shamba lililolimwa. (Kigiriki ni



*agros*- shamba ambalo ukulima unafanywa). Wangekuja kutoa heshima kwa Messiah usiku huo, lakini mamajusi waliwasili wiki kadhaa baadaye na kumpata Messiah katika nyumba (Mathayo 2:11). Malaika hawakutangaza kwa wachungaji kuzaliwa kwa Messiah kwa kuiba wimbo. Malaika walinena- malaika katika Biblia kamwe hawakuimba. Mwanafunzi wa dhati wa Biblia kila mwaka anatukanwa kusikia nyimbo za kr-smasi zikitangaza jinsi malaika waliimba wimbo!

Wakati mamajusi walifika Bethlehemu, Yahshua na wazazi wake waliishi katika nyumba (Mathayo 2:11). Hakuwa tena katika banda, ikiwa aliwahi kuzaliwa kwenye banda.(Hatuambiwi kuwa alikuwa, tunaambiwa tu alilazwa horini.)Hori lingekuwa malishoni.Yahshua aliye Messiah inavyowezekana zaidi alizaliwa katika kwenye hema nje nyanjani ambapo hori ndogo ilikuwa ya kulisha wanyama malishoni. Hori kama hiyo ilitumika kama kitanda kwa Messiah. Hakuna kutajwa kwamba alizaliwa katika banda la nyumba ya wageni, ni kuwa tu hakukuwa na chumba kwao katika nyumba ya wageni.

Katika mwezi wa Desemba, wachungaji walikuwa wameleta mifugo yao kwenye zizi kwa majira ya baridi kando ya Bethlehemu katika Nchi Takatifu. Wachungaji hawangekaa nyanjani, wakiangalia mifugo yao usiku, baada ya mwezi wa nane wa kalenda ya kimaandiko (Oktoba-Novemba), kwani hewa ingekuwa baridi na mvua baada ya Sikukuu ya Viwanda kawaida ikiwa katika mapema Oktoba.

Hadi siku hii watu wa Scotland wanaadhimisha Hogmanay katika majira ya baridi, neno linasemekana kutolewa kwa neno la Kifaransa cha zamani cha Norman, *hoguinane* sherehe ambayo zawadi za Mwaka Mpya zilitolewa au kubadilishwa kati ya marafiki. Kimila, karamu ya Hogmanay ilianza usiku wa manane kwa kuwasili kwa mgeni mrefu na mweusi. Muziki na vinywaji vya pombe zinajumuisha sehemu muhimu ya mila ya Hogmanay.

Lakini ni wapi sherehe ilianzia? Inapatikana kwa Biblia? Kweli, hakuna yoyote ya desturi, mila na sherehe zilizoambatanishwa kwa sikukuu za Krismasi/ mwaka mpya zinaweza patikana popote katika BIBLIA isipokuwa kwamba baadhi yazo zimelaaniwa kama kuwa ibada ya sanamu na upagani. Hogmanay kweli inakuja kutoka kwa neno la Kiebrania la sikukuu (hog- katika Kiebrania *chag* inamaanisha sikukuu, na *manay* ambayo inamaana ya nambari- *Mene*).Angalia Danieli mlango wa 5 ambapo sherehe ya pombe ilitolewa kwa Mene. Tafadhali chunguza Isaya65:11 kabisa kutoka kwa maandishi ya asili ambapo utapata wale wanaoacha Yahweh na kutunza amri Zake wanashika sikukuu za upagani. Moja ya hizi sikukuu ni kupatia sadaka ya kinywaji (pombe) kwa Mene. Desturi katika usiku wa Mwaka Mpya, watu wa dunia wanaenda sherehe, kucheza na kunywa kusherehekea kuwasili kwa mwaka mpya uliohesabiwa. (Ulijua kwamba maneno *money* (pesa) na mene yanawezafuatiliwa kwa mzizi mmoja? Uhusiano kama huo wa majina unamaanisha nini kwako?)

Moja ya kipengele cha kuchukiza zaidi cha sherehe ya Kr-smasi/Mwaka Mpya ni kutaka kwa watu kwa roho ya Kr-smasi (kutoka kwa chupa za vinywaji vya pombe). Katika sikukuu ya Kr-smasi watu wengi wanalewa, talaka nyingi hutokea, ajali mingi za magari kutokana na uendeshaji kwa waliolewa, na majanga mengi hutokea kuliko kipindi kingine chochote sawia kote mwakani. Majanga haya yanaungana na matumizi yasiyo na kiasi ya pombe. Dhahiri, aina hii ya roho ya kr-smasi ni mbaya- kutoka kwa Shetani na sio kwa Yahweh, baba wetu wa mbinguni, au kutoka kwa ambaye siku yake ya kuzaliwa inasemekena kusherehekewa- Messiah wa Israeli.

Miti ya kisasa ya kr-smasi inaweza kuua kama hauko mwangalifu. *Poinsettia*, *holly* na *mistletoe* inayo sumu ya kufisha, inayoweza kufanya mgonjwa au kuua mtoto

au mnyama-mdadisi vya kutosha kula majani. *Mistletoe*, mmea wa vimelea kwa asili uliteuliwa na Druids kama aina ya mti wa kufanya amani. Kubusu chini ya *mistletoe* ilielezewa kama mbingu ikifikia chini kubusu dunia kupitia kuzaliwa upya kwa mwana wa mbinguni (katika kugeuka kwa jua wakati mzunguko mpya unaanza). Hakuna yoyote ya mimea hii imetanjwa katika Biblia, bado inaheshimiwa karibu wakati wa kr-smasi.

### Wafanyabishara Wanafaidika na Udanganyifu!

Watu wengi wanaingia kwa undani kwenye deni kunua zawadi za kr-smasi, kitendo kisicho cha kimaandiko. Mamajusi hawakutoa zawadi mmoja kwa mwingine, lakini walileta kwa Mfalme aliyeteuliwa wa Yahweh, Yahshua aliye Messiah. Haingekuwa vyema kutoa utukufu kwa Yahshua kama walivyofanya mamajusi? Vyema bado, tunapaswa kutunza siku takatifu za Yahweh badala ya siku yoyote ya kuzaliwa.Lakini, kumbuka, siku ya kuzaliwa ya Yahshua ilikuwa labda siku ya kwanza ya Sikukuu ya Vibanda.

Miongoni mwa watu Waebrania, siku za kuzaliwa kamwe hazikutunzwa, sio vibaya mtu kumtakia mwingine siku ya kuzaliwa ya furaha, lakini kushiriki katika karamu za siku ya kuzaliwa na sherehe zingine inaweza kufuatiliwa moja kwa moja kwa upagani, haswa Ugiriki wa kale na Rumi.

Julius Sextus Africanus alikuwa mtu wa kwanza kutaja Desemba 25 kama siku ya kuzaliwa ya Yahshua. Kabla ya mwaka 225 C.E (Zama za Kawaida), kamwe haikutunzwa hivyo. Msimu wa baridi ulichaguliwa na Julius Sextus Africanus kama kuzaliwa kwa mwokozi kupitia uhusiano wake na matendo ya kidini ya upagani.

Ingeonekana kama mila mingi za Kr-smasi zimetolewa moja kwa moja kwa mpinga-messiah wa kale na mwokozi wa uongo, Nimrodi, na bibi-mama, Semiramis. Ulimwengu leo unaabudu Mwokozi wa uongo na mpinga-messiah chini ya kivuli ch ibada ya jua. Kurejesha ibada safi ya Biblia na kuondoa kutoka kwa maisha yetu sherehe na maadhimisho yachukizayo Mwenye-nguvu Yahweh inapaswa iwe lengo letu. Basi tusome Biblia na kuona kwetu jinsi isiyo na msingi zilivyo desturi zinazoambatanishwa kwa sherehe za Xmasi zinazotunzwa leo.

### Ukweli Unaokufanya uwe Huru!

Sasa kwamba umeona kweli mwenyewe, utatunza krismasi mwaka huu?

Sasa kwamba tumechunguza mila na desturi za sherehe za kr-smasi/Mwaka mpya na tumepata zimetolewa kwa mithiolojia ya kale ya upagani, utafanya nini binafsi? Tunapaswa kuendelea kuzitunza, vyovyote nusu-moyo tunaweza kuingia kwenye sherehe, sasa kwamba tumejua maadhimisho ni makosa?

Au tutafanya kama Yahshua aliye Messiah Mwenyewe ametuelekeza-KUTII Neno Lake na kutunza amri Zake (Mathayo 5:17-20)? Yahweh anatoa Roho Wake kwa wale pekee wanamtii Yeye (Matendo ya Mitume 5:32).

Wanaotunza amri za Yahweh watabarikiwa (Ufunuo 22:14). Wale hawatunzi hujilaani wenyewe (Kum. 27, 28).

Basi tusiongezee kwa Neno, au kupunguza, lakini tutunze amri za Yahweh kwa wema wetu (Kum. 6). Ondoa ambacho kinachukiza kwa Yahweh kutoka kwa ibada yako na upokee baraka zake leo.

Kwa nini usichukue mtazamo wa karibu kwa mafundisho ya Assemblies of Yahweh? Tunaweza kuthibitisha kuwa "njia ya maisha" tunayoenenda imeamuriwa na Neno la Yahweh. Ni nia yetu kutii Agano letu na Yahweh madhubuti kadri tuwezavyo.

Msimu huu wa sikukuu tazama gazeti na majarida kwa nakala ambazo moja kwa moja zinakiri asili ya upagani na maana ya mila na desturi zilizoambatanishwa kwa sherehe za kr-smasi. Tunapojua ni wapi mila na desturi hizi zilianzia, lazima tuzikatae kwa maisha yetu. Kisha lazima tutii Agano la Yahweh ili tumpendeze Yeye kama watoto watiifu.

Kwa maandishi zaidi ya kuelimisha juu ya somo la asili ya sikukuu za kidunia andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel, PA 19507. Unaweza kushangaa kwa desturi za dunia. Kumbuka maelezo ya Yahshua ya mwabudu wa kweli. ***"Ninyi mnaabudu msichokijua, sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi. Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Yahweh ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli."***(Yohana 4:22-24).

***"Lakini akamjibu akasema, imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo kinywani mwa Yahweh."*** (Mathayo 4:4).

**"Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyoijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Yahweh."** (Kumbukumbu la Torati 8:3).

Swali linabakia: Utatii? SNB



# Krismasi kama Biblia Inavyofundisha

**by Elder Jacob O. Meyer**

Kusanyiko la kimitume katika uzinduzi wake, lilianza kwa bidii kushahidia Ukweli wa ujio wa Messiah kwa dunia. Walichukua ujumbe huu katika maeneo ya mbali ya ulimwengu unaojulikana. Haswa aliyejitokeza alikuwa Mtume Paulo, ambaye alitimiza mengi kupitia safari zake za kuenda mbali, akihubiri kote katika Ufalme wa Kirumi.

Lakini maendeleo ya kushangaza sana yalifanyika. Watu wa kabila za kale hawangedumisha mafundisho safi! Watu wa upagani walichukua habari ya utu isiyo ya kawaida ya Messiah wa kweli wa Yahweh na kuingiza maisha Yake juu ya matendo yao na mila za upagani. Watu wa kidunia wanapendelea matendo yao ya upagani; hata hivyo wanataka wokovu pia.

Kwa kutelekeza bila sababu katika msimu wa Kr-smasi, watu wa ulimwengu wa Magharibi hutumia anasa, kwa zawadi ambazo hawawezi kumudu. Wanajiingiza



katika sherehe inayo- angazia vinywaji vya pombe.Wanasherehekea aina ya ladha za msimu. Vitendo hivi vyote vya kimila vinafanywa katika jina la kusherehekea siku ya kuzaliwa ya ambaye wanadai kuwa Mfalme wao. Kama jambo la kweli, kinyume ni kweli. Kupitia kwa mafundisho ya uongo, Messiah anakuwa wa chini kwa dhana zao wenyewe za binadamu. Yahshua aliye Messiah angeidhinisha mwenendo huru kama huo kusherehekea siku Yake ya kuzaliwa? Ni wazi hapana!

Mazoea ya kimila ya Ukr-sto wa kawaida kamwe hayapati msingi wa uanzishaji katika Maandiko. Taa zilizopambwa zinazoonyeshwa juu ya mti wa kr-smasi uliopambwa kwa rangi na kuangikwa kwa matawi ya kijani na *mistletoe* kamwe hazijatajwa katika Maandiko Matakatifu, zaidi kutoamriwa. Kufanya sherehe ya kichwa cha nguruwe, kutuma kadi za Kr-smasi, na kufanya misa usiku wa manane au huduma ya kanisa katika Desemba 25 haiwezi kupatikana popote katika Neno takatifu la Mwenye-nguvu Yahweh.

Kweli, mwanafunzi mwenye bidii wa biblia tayari anajua kwamba hakuna popote ndani ya kurasa za Biblia yetu unaweza kupata amri yoyote kutunza siku ya kuzaliwa, haswa hiyo ya Messiah.

Kama jambo la kweli, katika matukio matatu ambapo siku ya kuzaliwa imetajwa katika Biblia, kwa kila moja ya hafla hizo kifo katili kilitokea. Tafadhali thibitisha ukweli huu kutoka kwa Mwanzo 40:9-22, Ayubu 1:4 na 19, na Mathayo 14:3-12.

Kusherehekea kwa siku ya kuzaliwa ilikuwa isiyojulikana katika Uyahudi wa zamani, hivyo ni yakini kwamba Messiah kamwe hakusherehekea siku Yake ya kuzaliwa. Inavyoonekana, Mwenye-nguvu Yahweh hakutaka iwe ya kutunzwa; kwa sababu hiyo, tunaweza kwa urahisi kufahamu sababu ya kuacha kutaja kwa siku maalum katika Maandiko kwa siku ya kuzaliwa ya Messiah.

Wakati mwingi waandishi wataungama kikondoo kwamba Desemba 25 sio siku ya kuzaliwa ya Messiah. Je, ulijua kwamba ilikuwa zaidi ya miaka 200 baada ya kuzaliwa kwa Messiah kabla ya mtu yeyote kuweka Desemba 25 kama siku Yake ya kuzaliwa? Inavyoonekana, wa kwanza kuweka tarehe ya Desemba 25 kwa kuzaliwa kwa Mwokozi alikuwa Julius Sextus Africanus, mwanahistoria kutoka Alexandira, Misri, ambaye alijumuisha historia ya matukio ya ulimwengu hadi 221 C.E.Umetambua tarehe hiyo? Iliwachukua wanahistoria karne mbili na robo baada ya kuzaliwa kwa Messiah kuamua kwa tarehe ya Desemba 25 kama siku Yake ya kuzaliwa.

## Aliye Messiah Hakuzaliwa Desemba 25

Vifungu kadhaa vya kimaandiko vinathibitisha kwamba Messiah hangeweza kuwa amezaliwa katika msimu wa baridi, katika Desemba.

Geuka katika Biblia yako kwa Luka 1:5, Zakaria kuhani alikuwa mshiriki wa mkondo wa sehemu ya *AbiYah*. Kama tutahesabu sahihi, mimba ya Messiah ingewahi kuwa imetungwa karibu katikati mwa Desemba, badala ya kuzaliwa Desemba 25. Habari kama hiyo ni ya kushangaza sana unapogundua kwamba Luka alidokeza wakati wa kupata mimba ya Yohana mbatizaji kuwahi kutukia miezi miwili baada ya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa chachu, ambayo hufanyika katika majira ya machipuko. Mkondo wa AbiYah ulikuwa wa nane wa sehemu ya ukuhani kuhudumu katika Hekalu, 1 Mambo ya Nyakati 24:10. Makuhani hawa walihudumu wiki nane baada ya hitimisho ya majira takatifu ya Machipuko. Soma Luka 1, ukifuatia kila kutajwa maalum kwa wakati. Utagundua kwamba mimba ya Messiah ilitungwa miezi sita baada ya mimba ya Yohana.

*"Mvua ya kwanza inaanguka katika mwezi wa Marchesran, ambao unajibu kwa sehemu ya baadaye ya Oktoba na sehemu ya awali ya Novemba….Kutoka kwa wapi inaonekana [aliye Messiah] lazima azaliwe kabla ya katikati mwa Oktoba, kwani mvua ya kwanza ilikuwa bado haijakuja."* Kutoka **The Two Babylons**, Alexander Hislop, ukurasa 91-92.

Hapa tunagundua habari sahihi ya kihistoria iliyowekwa mbele na mwandishi wa kikweli. Uthibitisho mkubwa kwamba Messiah hakuzaliwa wakati wa ndani ya msimu wa baridi lakini kwa wakati wachungaji walikuwa wakichunga makundi yao uwanjani

karibu na Bethlehemu, unaweza kusoma katika Luka mlango wa 2.

Kimantiki, wakati pekee ambao unaweza kushughulikia ukweli wote wa ushahidi kuhusiana na wakati Mwokozi wetu alizaliwa ungekuwa msimu wa majani kupukutika wa mwaka. Mazao yalikuwa yamevunwa, watu walikuwa wanasafiri kwa Sikukuu ya Vibanda Yerusalemu kwa njia yoyote, hali ya anga ilikuwa nzuri vya kutosha kutoweka ugumu uliokithiri juu ya wanawake na watoto, na mapato yalikuwa kwa urahisi yaliyopatikana kulipa kodi ya Warumi. Hoja hizi zote zikiungana zinaelekeza mwanafunzi wa Biblia kuzingatia makini yake juu ya msimu wa vuli wa mwaka, karibu na siku za Sikukuu za mwaka za mwezi wa saba ambazo zimefanywa sheria katika Walawi 23.

Sio bahati tu kwamba tunapaswa kupata uthibitisho wa wakati wa msimu wa vuli kwa kuzaliwa kwa Messiah katika Yohana 1:14 ambapo **The Sacred Scripture** Bethel Edition inatafsiri: ***"Naye neno akawa mwili, akafanya vibanda miongoni mwetu, nasi tukaona utukufu wake, kama utukufu wa mwana wa pekee atokaye kwa baba, amejaa neema na kweli."***Yahshua aliye Messiah alichukua juu yake Mwenyewe uwepo wa binadamu. Alikuja kufanya vibanda (kuishi kwa muda) na familia ya binadamu aliyoteuliwa kuokoa.

Mara kwa mara katika msimu wa Sikukuu ya majira ya baridi tunagundua usawa dhahiri kati ya mila za Kr-smasi na Saturnalia ya Kirumi ya kale. Tunapoelewa kwamba maadhimisho ya kale ya Rumi yalisherehekewa karibu msimu wa baridi, uhusiano kati ya mila zinazohusiana na Kr-smasi kwa sikukuu za kale za upagani zinakuwa dhahiri zaidi.

Desemba 25 imesherehekewa kama sikukuu katika ibada ya upagani toka zamani. Kwa kweli, moja ya majina yaliyopewa msururu wa Saturnalia wa sherehe za kifalme katika mitholojia lilikuwa "paganalia!" Labda hii ndiyo asili ya jina "ibada ya upagani" ambalo mara nyingi linatolewa juu ya ibada ya aina yoyote ya uongo isiyo ya kimaandiko. Tafadhali angalia **Larousse's Encyclopedia of Mythology**, ukurasa 219.

Sherehe hii ya Saturnalia ilikuwa maarufu katika Rumi ya kale na ilituzwa kwa muda wa kuanzia siku tano hadi saba, kuanzia Desemba 17. Sherehe hii ya upagani ilikuwa na sifa ya sherehe isiyozuiliwa. Ilianza kwa sherehe ya kidini kumheshimu Saturn, ambayo ilifuatiwa na sherehe kubwa ya ulafi. Entimolojia ya jina *Saturn* inamaanisha *tele*.

Kutoka kwa **McClintock and Strong's Bible Cyclopedia**, nakala "kr-smasi," tunapata yafuatayo: Trynne anasema kwa njia yake ya nguvu (katika *histriomastiki*), "Bwana zetu wa utawa mbaya wa kr-smasi, pamoja na kucheza, barakoa, *mummeries*, wachezaji-jukwaa, na zingine kama hizi vurugu za kr-smasi, sasa katika matumizi na Wakristo, zilitolewa kutoka kwa Saturnalia ya Warumi, hizi na sherehe za Bacchanalia, ambazo zinapaswa kuwafanya Wakristo wote wachamuumba kuzichukia!"

## Sikukuu ya Ibada ya Jua-Desemba 25

"Chaguo la Desemba 25 labda ilishawishiwa na ukweli kwamba, katika siku hii, Warumi walisherehekea Sikukuu ya Kimithra ya M-ngu Jua (natalis solis invicti) na kwamba Sataurnalia pia ilisherehekewa karibu wakati huo." (nakala, "Christmas," **Collier's Encyclopedia**).

Yahshua aliye Messiah kamwe hakuzaliwa katika Desemba 25. Maadhimisho ya msimu wa baridi yalitolewa kabisa kutoka kwa ushirikina wa kale wa upagani. KR-SMASI KAMWE HAIJATA-

***Walipoona jua likipunguza mwendo wake kusini na kisha kusimama, wapagani waliamini kwamba maombi yao kwa jua yalikuwa yamefanikiwa.***



JWA KATIKA MAANDIKO. Kamwe haijatakaswa na Mwenye-nguvu Yahweh! Binadamu hawezi kuifanya takatifu, kwa njia yoyote hata watu wakitafuta kuitunza kwa bidii.

Katika kitabu chake **The Golden Bough**, Frazer anaonyesha kwamba Augustine na Leo Mkuu wote walielezea mbali dhana kwamba jua lilikuwa likiabudiwa, ingawa walikubali kimyakimya katika maandishi yao kwamba "Wakr-sto" wengi walikuwa wakihusisha neno Jua (SUN) na Mwana(SON).

## Upagani Kuiga Ukweli

Watu wa kale wa upagani waliona jua likisonga polepole kusini katika mbingu na siku ikikuwa ndogo. Kwa akili yao ya ushirikina waliamini kwamba jua lilikuwa likiondoka lisirudi kamwe. Kwa kutumia mapambo na sherehe za kidini waliamini ibada zao zingeshawishi jua kurudi.

Walipoona jua likipunguza mwendo wake kusini na kisha kusimama, wapagani waliamini kwamba maombi yao kwa jua yalikuwa yamefanikiwa. Wakati wa furaha isiyozuiliwa ulitokea. Sherehe na tafrija iliimarishwa. Unywaji wa vinywaji vya pombe uliinua msisimko.

Kisha, wakati wapagani waliona jua likisonga kaskazini tena, na wiki moja baadaye waliweza kuamua kwamba siku ilikuwa ikikua ndefu, mwaka mpya ulitangazwa. Watu wa kale walijulikana kupanda nguzo au mawe kwenye ardhi kuweka alama siku fupi zaidi na ndefu zaidi ya mwaka na jinsi jua lingesafiri kutoka kaskazini hadi kusini na kisha kaskazini tena (Stonehenge katika Uingereza kwa mfano).

## Mama na Mtoto

Katika sherehe ya Kr-smasi



kila mwaka, utatazama umbo la mama-na-mwana katika eneo la kuzaliwa, linalotumika mara nyingi. Karibu kila tamaduni ya upagani, hata hivyo, iko na rekodi ya kihistoria ya heshima ya mama na mwana. Mila hizi zinafuatilia nyuma kwa Nimrod, ambaye aliaminika kuwa amezaliwa tena kupitia mwana(son) wake mpya (sun- jua) Tammuzi.

Zaidi, kwa nini ufanye sanamu kutoka kwa eneo la kuzaliwa la mama na mwana, eneo la asili, kwa njia yoyote. Sio kuzaliwa kwa Yahshua aliye Messiah ambako kutatuokoa, lakini KIFO chake juu ya mti wa Kalvari na maisha yake ya haki ambayo aliishi kama mfano kwetu. Mtoto hawezi kuokoa ulimwengu, lakini mwenye haki, mwalimu wa Nazareti, mwenye nguvu lazima awe nahodha wa wokovu wetu, pamoja na damu yake ya patanisho.

## Miti ya Kr-smasi

Umewahi kushangaa juu ya sababu kwa nini mti wa msonobari unaletwa kwenye nyumba wakati wa Kr-smasi na kupambwa na mwanga unaong'aa na taa? Hakuna popote unaweza kupata amri kufanya hili katika Biblia. Mila hii ya wapagani pia inatokana kwa ibada ya Nimrod, na Biblia kweli inakataza mila hiyo!

Wakati Nimrodi aliuawa na Shemu (mwana wa Nuhu) kwa uasi wake dhidi ya Mwenye-nguvu Yahweh na Ufalme Wake unaotawala, Nimrod alionyeshwa katika Mitholojia kama mti uliokufa ambao ulikuwa umekatwa. Mitholojia ilimwonyesha akiwa na ishara ya nyoka, *Aescalapius* (mrejeshaji wa maisha), ambayo ilijisokota kuzunguka kisiki kilichokufa. Kando ya kisiki kilichokufa mti mpya ulichipuka kwenye uzima kutoka kwa mizizi iliyokufa. Kweli, lazima tukumbuke kwamba nyoka katika Biblia inasimamia Shetani ibilisi, Ufunuo 12:9 na Mwanzo mlango wa 3.

Mitholojia hii ya upagani (mti uliokufa na shina mpya) inaonyesha jua linalokufa, na jua jipya lililorejeshwa kwa fahari katika Desemba 25 kila mwaka.



## Kuabudu Mti Kunalaaniwa

Basi tusikie Mwenye-nguvu Yahweh akiongea kwetu katika Yeremia 10:2-8 ***"Yahweh asema hivi, msijifunze njia ya mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo.***



***Maana desturi za watu hawo ni ubatili, maana mtu mmoja hukata mti mwituni, kazi ya mikono ya fundi na shoka. Huupamba kwa fedha na dhahabu, huukaza kwa misumari na nyundo, usitikisike. Mfano wao ni mfano wa mtende, kazi ya cherahani, hawasemi; hawana budi kuchukuliwa, kwa sababu hawawezi kwenda. Usiwaogope; kwa maana hawawezi kutenda uovu, wala hawana uwezo wa kutenda mema. Hapana hata mmoja aliye kama wewe, Ee Yahweh, wewe ndiwe uliye mkuu, na jina lako ni kuu katika uweza. Ni nani asiye kucha wewe, Ee mfalme wa mataifa? Maana hii ni sifa yako wewe; kwa kuwa miongoni mwao wenye hekima wote wa mataifa, na katika hali yao ya enzi yote pia, hapana hata mmoja kama wewe. Lakini wote pia huwa kama wanyama, ni wapumbavu. Haya ni maelezo ya sanamu, ni shina la mti tu."***

Mwabudu wa Kweli lazima kamwe asiwe mwenye hofu kwa mabadiliko ya misimu au ishara zingine katika mbingu kama waabudu wa upagani. Lazima tumtumikie Yahweh na kumtii kwa kutunza amri zake, kumwamini Yeye kwa wokovu. Kamwe tusiwe wajinga na kuzorota katika kufikiria kwetu kwa kuabudu kiumbe badala ya muumbaji (Warumi 1:25). Tutamtumikia Mfalme aliye na Nguvu wa ulimwengu, Yahweh Elohim, na kumwogopa Yeye na Mwana Wake kama Muumbaji wa vyote.

## Shada la X-masi

Zikitengenezwa kutoka kwa kijani kibichi, shada la maua mara nyingi ni duara. Kijani kibichi inamaanisha maisha ya milele, uwepo usio kufa kamwe katika mitholojia ya upagani. Umbo mduara linaashiria jua, jinsi lifanyavyo halo katika sanaa za kawaida za kidini.Kwa sababu hiyo, shada mduara za Kr-smasi zinasimamia jua la milele, lisilo kufa kamwe, au jua linalojifanya upya. Kwa ziada, umbo mduara pia linaweza kuhusiana na ishara ya kike ambayo inasimamia kwa kuzaliwa upya kwa maisha. Ishara kama hizo zinaonekana kote katika sanaa za Ukristo na zilinakiliwa kutoka kwa dini ya kale ya Kikanani. Tafadhali soma Hesabu 25, miongoni mwa vifungu vingine.

Sisi, ambao tungekuja kutoka Babeli, lazima tuondoe upagani kama huo kutoka kwa maisha yetu,kama yanayowekwa kwa kumbukumbu katika sanaa za kidini na ishara za sikukuu za upagani. Lazima tuondoe hayo yote ambayo pengine yanaweza kumkasirisha Baba wetu wa Mbinguni.




## Roho ya Kr-smasi?

Tabia ya kusherehekea Krismasi ni wakati wa kunywa (roho ya krismasi). Wakati wa Sikukuu za msimu wa baridi ni muhimu kwamba kila mtu anayejihusisha katika sherehe hiyo anywe kinywaji cha pombe. Chupa mingi za vinywaji vya pombe zinapewa kama zawadi ya kr-smasi. Mara nyingi kunywa katika roho iliyo kwenye chupa inaelekeza kwa janga.

*"Sikukuu kama ilivyowekwa na Caligula, ilidumu siku tano, hatamu zilizolegea zilitolewa kwa ulevi na tafrija (saturnalia). Hili lilikuwa kwa usahihi njia ambayo, Berosus, sherehe ya ulevi ya mwezi wa Tebeti inayojibu kwa Desemba yetu, katika maneno mengine, sherehe ya Bacchus, ilisherehekewa katika Babeli....Wassailing bowl ya Kr-smasi ilikuwa na mwenzake sahihi katika "sherehe za ulevi" za Babaeli, na maadhimisho mengine mengi bado yanatunzwa miongoni mwetu katika Kr-smasi zinakuja kutoka kwa maeneo sawa kabisa."* **The Two Babylons**, na Alexander Hislop, ukurasa 96-97.

Ni wapi katika maandiko unaweza kupata kifungu kikiunga mkono kunywa vinywaji vya pombe na wenzako katika sherehe ya Kr-smasi? Unaweza kufikiria Mitume wakifanya sherehe ya Ofisi kusherehekea siku ya kuzaliwa ya Messiah? Bila shaka hakuna Maandiko yanaweza kupatikana ambayo hata kwa umbali yanadokeza kwa mwenendo huru kama huo miongoni mwa Mitume, ambao lengo la umoja katika maisha lilikuwa kutimiza

*Continued on page 20.*



# THE LAW OF YAHWEH

# Amri ya Nane

# Usiibe

Na Mzee Jacob O. Meyer

*"Lakini wana wa Israeli walifanya dhambi katika kitu kilichowekwa wakfu; maana Akani mwana wa Karmi, mwanawe Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila ya Yuda, alitwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu: hasira ya Yahweh ikawaka juu ya wana wa Israeli.*

*"Kisha Yahshua akawatuma watu kutoka Yeriko mpaka mji wa Ai, ulio karibu na Bethaveni, upande wa mashariki wa Betheli, akawaambia, akisema, pandeni juu mkaipeleleze nchi, basi wakapanda juu wakaupeleleza Ai. Wakarejea kwa Yahshua wakamwambia, wasiende watu wote, ila waende watu kama elfu mbili, tatu, wakaupige Ai; usiwataambishe watu wote kwa kuwaendesha huko; maana watu hao ni wachache tu. Basi watu wakaenda huko wapata elfu tatu tu: nao wakakimbia mbele ya watu wa Ai. Watu wa Ai wakawapiga watu kama thelathini na sita; wakawafuatia kutoka mbele ya mlango mpaka Shebarimu, wakawapiga huko kwenye matelemko; mioyo ya watu ikayeyuka, ikawa kama maji.*

*"Yahshua akararua mavazi yake, akaanguka kifudifudi mbele ya sanduku la Yahweh hata jioni, yeye na wazee wa*

**Katika nyakati zetu za kisasa, tunaishi katika jamii ambayo dhahiri imeendeleza viwango viwili. Ni wazi watu wamekuja kufikiria kwamba sheria inashikilia mamlaka tu juu ya watu wengine. Mradi tu mtu anaweza kuponyoka kwa kufanya vibaya, hata kuvunja sheria, inachukuliwa mwenendo unaokubalika.**

*Israeli; wakatia mavumbi vichwani mwao. Yahshua akasema, ee Mwenye-enzi Yahweh, kwa nini umewavusha watu hawa mto wa Yordani, ili kututia katika mikono ya Waamori, na kutuangamiza? Laiti tungelikuwa radhi kukaa ng'ambo ya Yordani, Ee Yahweh, niseme nini baada ya Israeli kuwapa visogo adui zao! Maana Wakanani na wenyeji wote wa nchi hii watasikia habari hii nao watatuzingira na kulifuta jina letu katika nchi: nawe utafanya nini kwa ajili ya jina lako kuu?*

*"Yahweh akamwambia Yahshua, Haya!Inuka; mbona umeanguka kifudifudi hivi? Israeli wamefanya dhambi, naam, wamelivunja agano langu nililowaagiza; naam, wametwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu, tena wameiba, tena wameficha na kuvitia pamoja na vitu vyao wenyewe. Ndiposa Wana wa Israeli hawawezi kusimama mbele ya adui zao; wakawapa visogo adui zao.Kwa sababu wamelaaniwa: mimi sitakuwa pamoja nanyi tena, msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu. Haya! Inuka, uwatakase watu, ukaseme, Jitakaseni, mwe tayari kesho; maana Yahweh Elohim wa Israeli, asema hivi; kitu kilichowekwa wakfu kiko katikati yako, Ee Israeli; huwezi kusimama mbele ya adui zako, hata mtakapokiondoa kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu. Basi asubuhi mtaletwa karibu nami, kabila kwa kabila; kisha itakuwa ya kwamba, kabila ile atakayoitwaa Yahweh, itakaribia jamaa kwa jamaa na jamaa ile atakayoitwaa Yahweh itakaribia nyumba kwa nyumba; na nyumba ile atakayoitwaa Yahweh, itakaribia mtu kwa mtu. Tena itakuwa ya kwamba, yeye atakayetwaliwa naye anacho kitu kile kilichowekwa wakfu, atateketezwa kwa moto, yeye na vitu vyote alivyo navyo; kwa sababu amelivunja agano la Yahweh, na kwa sababu ametenda upumbavu katika Israeli.*

*"Basi Yahshua akaondoka asubuhi na mapema, akawasongeza Israeli kabila kwa kabila; kabila ya Yuda ikatwaliwa. Akazisongeza jamaa za Yuda, akaitwaa jamaa ya Wazera; akaisongeza jamaa ya Wazera mtu kwa mtu; Zabdi akatwaliwa. Akawasongeza watu wa nyumba yake, mmoja mmoja; na Akani, mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila ya Yuda akatwaliwa. Yahshua akamwambia Akani, Mwanangu nakusihi, umtukuze Yahweh, Elohim wa Israeli, ukaungame kwake; uniambie sasa ulilolitenda, usinifiche. Akani akamjibu Yahshua, akasema, Kweli nimefanya dhambi juu ya Yahweh, Elohim wa Israeli nami nimefanya mambo haya: Nilipoona katika nyara joho nzuri ya Babeli, na shekel mia mbili za fedha, na kabari ya dhahabu, uzani wake shekel hamsini, basi nilivitamani, nikavitwaa; tazama, vimefichwa mchangani katikati mwa hema yangu na ile fedha chini yake.*

*"Basi Yahshua akatuma wajumbe wakapiga mbio mpaka hemani, na tazama, vile vitu vilikuwa vimefichwa hemani mwake; na ile fedha chini yake. Wakavitoa kutoka hapo katikati ya hema, wakavileta kwa Yahshua, na kwa wana wa Israeli wote, nao wakaviweka chini mbele ya Yahweh. Kisha Yahshua, na Israeli wote pamoja naye wakamtwa Akani, mwana wa Zera na ile fedha na lile Joho, na ile kabari ya dhahabu na wanawe, na binti zake na ng'ombe zake, na punda zake, na kondoo zake, na hema yake, na vitu vyote alivyokuwa navyo, wakavileta juu hata mbonde la Akori. Yahshua akasema, Mbona umetufadhaisha hivi? Yahweh atakufadhahisha wewe leo. Ndipo Israeli wote wakampiga kwa mawe, kisha wakawateketeza kwa moto na kuwapiga kwa mawe. Kisha*

***wakakusanya juu yake chungu kubwa ya mawe hata leo; naye Yahweh akauacha ukali wa hasira yake. Kwa sababu hiyo jina ya mahali pale ikaitwa Bonde la Akori, hata hivi leo."*** (Yahshua 7:1-26).

Leo tutazingatia juu ya mada ya amri ya nane, inayopatikana katika Kutoka 20:15, ***"Usiibe."***

Kama tu amri mbili za awali, hii pia ni fupi sana na kwa uhakika. Inajumuisha amri ambayo ni vigumu kueleweka vibaya, lakini leo inaonekana kuwa moja ya amri inayokiukwa sana mara kwa mara. Katika Biblia ya Kiebrania, inaonekana kama maneno mawili tu (kitenzi na sehemu hasi).

Katika nyakati zetu za kisasa, tunaishi katika jamii ambayo dhahiri imeendeleza viwango viwili.Ni wazi watu wamekuja kufikiria kwamba sheria inashikilia mamlaka tu juu ya watu wengine. Mradi tu mtu anaweza kuponyoka kwa kufanya vibaya, hata kuvunja sheria, inachukuliwa mwenendo unaokubalika. Biblia inabainisha sababu ya mzizi wa uhalifu wote na vurugu tunayoiona imeenea katika Marekani leo. Wimbi hili la uhalifu linazidi kwa mbali asilimia ya ongezeko katika idadi ya watu, na inatoka kutoka kwa kipengele cha msingi cha tabia ya binadamu ya kupenda mali na ubinafsi. Walimu, maafisa wa serikali, watendaji wa magazeti na viongozi wa kidini na biashara kote Marekani wamepiga kelele kuonya taifa letu, na ulimwengu, kwa hatari inayopanda ya uhalifu na vurugu. Hata hivyo, kiwango cha uhalifu kinapanda! Watu wachache kweli wanasikia onyo, wakipendelea kuhamisha lawama kwa wengine.

Mtu wa kawaida atasisitiza wakati huu, "Vizuri huwezi maanisha mimi. Siendi na kuibia benki," au "Sikughushi vitabu vya shirika yoyote na kuiba maelfu ya dola. Siibi!" Mtu wa kawaida anaweza kusema, "Hata sikufanya wizi wa duka yoyote." Walakini, kuiba inaweza kuelezwa kama kanuni ya kujitwalia chochote ambacho si chako halali.

Basi kwa uangalifu tuchunguze amri ya nane kwa jicho la uchambuzi. Inasema nini? Mwokozi, Yahshua aliye Messiah, alikuja kukuza Sheria ya Yahweh na kuifanya ya kuheshimiwa, tukufu zaidi, kama baadhi ya tafsiri zinavyotoa Isaya 42:21. Akili ya kimwili inaweza tu kuona juu juu nini ni wazi kwa uso kwa macho ya binadamu, wakati macho ya kiroho yanapenya kwa undani kuelewa mambo yaliyofichwa na inapata mambo mapya katika Neno la Yahweh.

Wazo hili linaonyeshwa kikamilifu hivyo katika 1 Wakorintho 2:10. ***"Lakini Yahweh ametufunulia sisi kwa Roho: maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Yahweh."***Katika mstari wa kumi na nne tunasoma, ***"Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Yahweh; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawawezi kuyafahamu kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya roho."***

Kote katika Maandiko Matakatifu, tunapata uenezi kwa amri hii ya kutochukua kwa umilikaji wa kibinafsi wa nini ni ya mtu mwingine, nini mtu mwingine labda amefanyia kazi kwa ugumu kupata. Walawi 19:11 inaweka mbele maagizo maalum kwa Waisraeli ambayo yanaweza pia kutumika kwa usawa zaidi kwa Waisraeli wa kiroho wa siku za kisasa. **"Msiibe; wala msidanganyane, wala msiambiane uongo."** (Tafadhali soma Walawi 19, ukizingatia jinsi ulimwengu ungebadilika sana kwa ubora kama amri hizi zingetiiwa kwa uaminifu.)

Tumeshuhudia, katika nyakati zetu kashfa za kutisha kwa mfano katika jamii ya kibiashara, kupanga bei miongoni mwa baadhi ya kampuni kubwa. Lakini watendaji wa biashara hao hawajaonyesha maumivu yoyote ya dhamiri (inaonekana) kwa kutenda kwa uongo kwa watu wenzao, wengi wa wateja wao wakitoka kwa darasa la masikini wa nchi ambao pengine, hata hawapati wapasavyo kupata hata kujikimu kwa kawaida kwa familia zao.

Pia, ni mara ngapi umesikia hadithi za watu waliodanganywa kwa ununuzi wa gari mbovu au muuzaji wa vifaa vya nyumbani, wafanyabiashara wanaopotosha bidhaa fulani ambazo walikuwa wanajaribu kupakua juu ya umma usiotarajia? Wale waliodanganywa kwa njia hiii wamekuja kupitia maana ya mithali ya zamani, "Mnunuzi awe na tahadhari." Najua kuhusu sheria chache kwenye vitabu kuwalinda watu wasio na hatia waliopatikana katika shida kama hiyo, na bado katika Kitabu cha Vitabu inaonekana Sheria inayoshughulikia hali hii haswa. Walawi 19:13 inasema karibu wazo sawa kabisa.***"Usimdhulumu jirani yako, wala kumnyang'anya mali yake; ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi."***

Luka 6:38 pia inaweka nje dhana hii ya haki ya kufanya biashara, iliyotolewa kwetu na Mwokozi wetu, Yahshua aliye Messiah. ***"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa."***

Ulimwengu huu ungekuwa wa ajabu vipi kama dhana hii tukufu ya sheria ya kiroho dhidi

ya kulaghai au kudanganya jirani ya mtu ingetiiwa katika ukuzaji wake wote wa kiroho. Wafanyakazi wangekuwa na hamu ya kufanya kazi nzuri ya siku kwa mshahara wa haki wa siku. Wafanya kazi wangependezwa, na kuzingatia sana na kutengeneza bidhaa ya ubora wa hali ya juu, na kuwa na wasiwasi kutengeneza bidhaa zenye "kasoro sifuri." Sio tu katika Marekani, lakini kote duniani leo, mtazamo ni wazi kwamba mradi tu tunatoa bidhaa za kuuzwa, si jambo zinafikia mnunuzi katika hali gani, au ni ya kudumu namna gani.

Wiki kadhaa zilizopita jarida kubwa la habari la Marekani lilichapisha nakala, iliyoonyesha kwa umaarufu ikichambua shida za wazalishaji kuhusiana na uzalishaji wa bidhaa ambazo zitafikia kiwango kwa watumiaji wanaohitaji wa umma. Walibainisha mtazamo wa kawaida na usio na wasiwasi wa waajiriwa wao kama chanzo kikuu cha shida zao. Wafanyakazi wa uzalishaji wana wasiwasi zaidi kuhusu urefu na marudio ya mapumziko ya kahawa, au mapenzi ya nje ya ndoa kiwandani, na hawazingatii katika kufanya kazi yao. Tunapata kwamba Suleimani, katika Mhubiri 5:19 anawaambia wasikilizaji wake kufurahia katika kazi yao.

Nilipokuwa kijana nikikuzwa shambani, babangu alinituma kwa jirani kununua pishi kadhaa za mbegu ya ngano kumaliza kupanda shamba. Tulipoenda ghalani na akaanza kupima mbegu, mtu huyu alifuata Maandiko wazi, kwa sababu alichukua kipimo cha nusu pishi na kukijaza, na kisha akakitikisa, lakini kisha akafanya laini juu kwa ubao wa kunyoosha. Nilistaajabu kwa hili kama analifanya mara nne katika kujaza mfuko wangu kwa pishi mbili za mbegu. Walakini, tulipopima pishi zile mbili na mfuko ulikuwa karibu kujaa alichota mbegu zaidi kutoka kwa pipa na kipimo chake na kuendelea kujaza mfuko hadi kujaa, akibakisha nafasi tu ya kufunga mfuko kwa kamba juu. Alitabasamu kwangu na kutoa maoni "hata kumwagika, hiyvo ndivyo Maandishi yamesema!"

Watumishi na wanafunzi wa Biblia wanaweza pia kuwa na hatia ya kuiba. Geuka nami kwa Yeremia 23:30-31. ***"Basi kwa sababu hiyo mimi ni juu ya manabii hao, asema Yahweh, WANAOIBA kila mtu jirani yake maneno yangu. Tazama, mimi ni juu ya manabii, asema Yahweh, wanaotumia ndimi zao kusema, yeye amesema."*** Tumeonywa na Maandiko Matakatifu kuamini tu nini Biblia inatuambia kuhusu njia kwa wokovu. Wakati mwingi watu wanaweza kuwa na hatia ya kufanya dhambi dhidi ya Yahweh kwa kuamini nini mtu mwingine anatuambia ni ukweli kuhusu Biblia, wakati kwa kweli sio Ukweli.

Mara nyingi, hatua ya mafundisho iliyo katika ubishani miongoni mwa ndugu inaweza kusafishwa kwa kusoma mistari inayoizunguka na kupata muktadha. Kaka mzee katika Imani mara moja alianiambia, "Jua nini unazungumzia kuhusu wakati wote. Shikamana na muktadha, na kamwe hutakosea. Maandishi yoyote yaliyochukuliwa nje ya muktadha ni kisingizio kwa mafundisho ya uwongo!"

Huu ni ushauri mzuri kufuata. Tuna uwajibikaji kwa wokovu wa roho zetu wenyewe. Lazima tujue, nini sisi wenyewe tunaamini kuhusu Biblia.Kile mtu mwingine anaamini kuihusu hakiwezi kamwe kutuokoa. Hakika tutapokea adhabu iliyoelezewa kwa mwisho wa zama ikiwa tutaendelea katika kufuata watu ambao hawafanyi lolote ila kuiba maneno kutoka kwa jirani yao au kupotosha Neno la Yahweh. (2 Petro 3:16).

Katika Maandiko tuliyosoma mwanzoni mwa nakala hii (tukio la Akani), tunapata kwamba majeshi ya Waisraeli walikataliwa ushindi vitani dhidi ya mji wa Ai. Ulikuwa kweli mji usio na maana na wenyeji wachache, ukilinganishwa kwa miji mingine ya Wakanani, miji na vijiji bado kushindwa. Wazee walipouliza kwa Yahweh kuhusiana na sababu ya kushindwa, Mwenye-nguvu Yahweh aliwaambia kwamba kulikuwa na dhambi kambini. Mtu fulani alikuwa ameiba vitu kwake mwenyewe kutoka kwa vita vya awali na kuzificha. Hizi zilikuwa joho ya Babeli, idadi ya sarafu za fedha na kabari ya dhahabu. Lazima tuelewe kwamba hatuwezi kuingiza chochote kutoka ibada ya upagani kwenye mioyo yetu.

Yahweh anasema katika mstari wa 11, kwamba Akani alikuwa ameiba vitu hivi, na anasema katika mstari wa 15 kwamba mtu fulani alikuwa ameasi (au kuvunja) Agano, Sheria ya Yahweh. Akani ilibidi alipe sadaka kuu ya maisha yake kwa kutotii huku kwa Sheria ya Yahweh- kifo kwake mwenyewe na wapendwa- adhabu ya dhambi chini ya Sheria. Angalia pia Warumi 6:23.

Leo hatufungwi tena na Sheria ya adhabu ya kutoa sadaka. Hata hivyo, tunahitajika kutii Sheria ya kifalme ya upendo.Tunahitajika kutii Sheria ya Yahweh ya uhuru. Sheria ya Agano ya utiifu, amri 10 ya sheria ya maadili, pamoja na sheria na hukumu zinazohusiana nazo, ni zetu kutii katika wakati wetu. Ulimwengu wa ajabu namna gani huu utakuwa wakati mataifa yote yatajifunza haki (matumizi-sahihi), wakati watajifunza kutii Sheria ya Yahweh kama ilivyotabiriwa katika mlango wa pili wa Isaya na Mika mlango wa nne. Unaishi maisha ya utiifu wa

kujitolea kwa Sheria za Yahweh itakayokuletea maisha ya milele?

Kumbuka kutii na kuishi kweli kwa yale Maandishi yanatuagiza kufanya. Katika Warumi 6:23 tunapata, ***“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Yahweh ni uzima wa milele katika Messiah Yahshua Mkuu wetu.”*** Gharama kidogo vipi kulipia kwa zawadi kubwa katika mwisho wa maisha yetu ya binadamu: imani katika Messiah Yahshua na utiifu kwa Baba wetu wa mbinguni. Lisifu Jina lake milele!

Basi tusisahau kwamba njia nyingine watu leo wanaiba kwa Yahweh imeelezewa katika Malaki mlango wa 3. ***“Je, Mwanadamu atamwibia Elohim? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kuwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Yahweh wa majeshi; kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Yahweh wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Yahweh wa majeshi.”***

Nitakuacha na wazo hili katika Waefeso 4:28. ***“Mwibaji asiibe tena: bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.”***

Kisha tuwe kama Zakayo katika Luka 19, aliyepitia mazungumzo ya kina ya kweli yenye msingi wa urejeshaji.

Basi tuchukue mfano wa Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wetu mpendwa mbinguni, unaoelezea anayetoa na zawadi. ***“Kwa maana Yahweh aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”*** (Yohana 3:16).

Na tuweze kuiga Baba wetu aliye mbinguni na kuwa wakarimu badala ya kupenda mali, kudai kupata.

“Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa



# Jena Matawi Yanaanguka

Vuli nyingi maishani mwangu, nimetazama misimu ikibadilika, Tuliona nyakati za kulima na kupanda, mavuno yanapita, majira yakaisha.
Kuketi katika bustani inayo pendeza sana, baada ya baridi kugusa miti,
Majani yanaanguka, yakipepea kwa upole kuelekea ardhini,
ikiwa na rangi angavu nayo brashi ya mbinguni na rangi.
Upepo laini unavuma, ghafla majani yanaachia mshiko wao,
kutoka kwa tawi huanguka kidogo,
Na kuweka zulia laini, na kuunda mifumo ya rangi ya vuli chini.
Majani yanaanguka, O,
jinsi maisha yameisha kwa wote,
hapo kwa kipindi kifupi tu,
Sasa upepo laina unavuma, na wanaanguka
kuelekea ardhi.
Maisha ni kama majani, bila kufikiria, tunapuuza w
akati wa kijani kibichi! Hivi karibuni mwisho wa maisha unakaribia, msimu wa baridi unakuja, tunateleza mbali, Imesahaulika hivi karibuni, ni hatima yetu.

*"Naam, mtu akiishi miaka mingi, na aifurahie yote; Lakini naazikumbuke siku zijazo za giza, kwa maana zitakuwa nyingi. Mambo yote yajayo ni ubatili."*

~MHUBIRI 11:8

BY ELDER JACOB O. MEYER

# *Krismasi* kama Biblia Inavyofundisha

*Continued from page 13.*

Utume Mkuu.

### Santa na Kulungu Wake

Ni wapi mtu katika suti ndogo nyekundu, ambaye anawakilisha Roho ya Kr-smasi, alitoka?Aliitwa Mtakatifu (?) Nikolao, iliyofupishwa kwa St. Nick! Umewahi kuzingatia "Nick" ni nani kweli? Ni jina la utani la Shetani Ibilisi! Thibitisha ukweli huu kwako mwenyewe kutoka kwa kamusi nzuri.

Kwa nini wazazi wawaambie watoto uongo kama hadithi ya Santa Klausi katika wakati wa Kr-smasi? Udanganyifu katika kuwaambia watoto kwamba mtu ndogo anayeitwa Santa Claus (ST. Nicholus) atacha zawadi chini ya mti ni ulaghai ambao kisaikolojia utaharibu watoto.

Santa Clausi ana umaarufu wa kuwahi kuwa ufupisho wa jina Saint Nicholas. Walakini, kutoka kwa uchunguzi, ukweli wa ajabu unajitokeza. Kidogo kinajulikana kuhusu huyu mtakatifu kutoka kwa karne ya nne. Nikolao anatajwa katika Matendo ya Mitume 6:5, ambapo aliteuliwa mmoja wa mashemasi wa kwanza, lakini hakuna chochote kinajulikana kumhusu isipokuwa kwamba anaelezewa kama mwongofu. Katika **Webster's New World Dictionary** tunasoma, "*Mtakatifu wa 4, karne ya 4 A.D; Askofu wa Myra; Mtakatifu patron wa urusi, wa Ugiriki, na wa watu wachanga, mwanamaji na kadhalika; siku yake ni Desemba 6; cf. SANTA CLAUS.*" Mtu anaweza kwa urahisi kufunga ndani jina Wanikolai hapa.

Wachambuzi wanadai kwamba hili lazima lilikuwa dhehebu la kuasi lililoanzishwa na Nikolao (labda aliye kwenye Matendo ya Mitume au mwingine), lakini wanakubali rahisi kwa kutokuwa na uhakika kwao. Kwa kuangalia leksikoni tunasoma kwamba **Strong's Exhaustive Concordance** inaiorodhesha kama #3531 (**American Standard Version** ya 1901 ilisahihisha maendelezo kwa Nicolaitans). Kisha neno linafuatiliwa kwa #3534, *Nikos*. Kama hili ni kweli (na hakuna sababu kutoiamini), basi mzizi wa neno "Nikolao" ni Nike. Sehemu ya mwisho ya neno basi ingekuwa #2992, *Laos*, watu.

Basi tukumbuke pia kwamba neno Wanikolai, Ufunuo 2:9 na 3:9, ilikuwa fundisho LINALOCHUKIWA na Yahshua aliye Messiah na mwenye-nguvu Yahweh Baba wetu wa mbinguni.

Nike alikuwa nani? Neno Nike linaweza kuunda msingi wa neno Nicholas. Alikuwa mshindi wa upagani mwenye mabawa, mwinjilisti wa Zeus. Mara mingi Nike anaweza kuonekana leo akionyeshwa kwenye vikombe hata katika wakati wetu wa kisasa. Liangalie, Santa Claus, St. Nicholas, au St Nick, analeta zawadi kutangaza ujio wa kuzaliwa kwa Y-su Kr-sto. Ni wazi, kunao uhusiano wa ajabu wa karibu sana hapa na upagani.

### Mababa Mahujaji Walikataa Kr-masi

Wengi wa wahamiaji wa asili walikuja kutoka Ulimwengu Mpya na nia ya kuanzisha tena Imani ya kweli ya Yahshua aliye Messiah, na Imani ya Mitume nje ya mateso ya papa wa Kirumi. Baba mahujaji, ambao walikuwa kimsingi wapuritani, walikuja kwa Ulimwengu Mpya katika tarehe ya mapema (1620) na kukaa katika New England. Ilikuwa nia yao kumtumikia Baba wa Mbinguni na Yahshua aliye Messiah katika Roho na Kweli.

Nukuu ifuatayo ni kutoka kwa **Encyclopedia Britannica, 11th Edition**: "Katika 1644 wapuritani wa Kiingereza walikataza kushangilia au vitendo vya kidini vya aina yoyote kwa kitendo cha bunge, kwa msingi kwamba ilikuwa sherehe ya upagani, na kuiamuru kuwekwa kama saumu. Charles wa 2 alihuisha sikukuu, lakini Scots walizingatia kwa mtazamo wa wapuritani."

Kwa kweli, kwa karne, ibada ya kweli ya kimessiah kamwe haikuwa kubwa au pana. Kila mara ilijumuishwa na watu wachache, labda mmoja au watu wawili au familia, ambao walitafuta kwa bidii kumtumikia Yahweh na kukataa kwa uhusiano na ibada ya sanamu au ibada ya uongo. Kidogo sana kimesikika kutoka kwao kupitia kwa ripoti za wanahistoria wa ulimwengu. Lakini, hata hivyo, makundi madogo mara kwa mara, kama vile Wanazarayo, *Waldenses* na Baba wahujaji, hawafanyi vichwa vya habari vya kihistoria.

Kwa nini watu katika nyakati za kisasa wanaendelea kushikilia kwa uaminifu kwa mila ambazo zilitolewa kutoka kwa ushirikina wa kale wa upagani? Kwa nini kamwe hawaulizi swali wapi zilitoka? Kwa nini usisome Biblia na kutii Maandiko Yaliyoongozwa badala ya kujaribu kuunga mkono maadhimisho ya jadi, yasiyo ya kimaandiko kwa Maandiko Matakatifu. SNB



## Mwelekeo wa Kinabii

# Nakala ya Sanduku Mpya Yafichuliwa



Juu: Mfadhili wa mradi Lewis Topper azindua nakala ya Sanduku la Agano huko Yerusalemu mnamo Oktoba 20, 2024. Picha na Alex Traima
Hapa chini: Taswira ya nguzo ya wingi na moto.



*"Mfano wa Sanduku la Agano, lililojengwa kwa ustadi, waundaji wake wamesema, kwa maelezo ya torati ya chombo kitakatifu kilichokuwa cha Hekalu la Kwanza, cha katikati ambacho kilionyeshwa huko Yerusalemu Jumapili jioni, wakati wa siku za kati za sikukuu ya Sukkot.*

*"Sanduku lililoelezewa katika Torati, ambalo lilikuwa na mawe ya Amri Kumi kati ya vitu vingine vitakatifu, lilifichwa baada ya uharibifu wa Hekalu la Kwanza, kulingana na mapokeo ya marabi," kama ilivyoripotiwa na Alex Traiman katika JNS.org.*

*Likiundwa kutoka kwa mbao zilizochaguliwa kutoka kwa mbao za mshita na kufunikwa kwa dhahabu iliyotolewa,mfano wa safina ulikusanywa bila viungio vya mitambo.*

*Je! Sanduku hii itakuwa katika-Hekalu la Tatu ambalo litajengwa upya hivi karibuni?*



Juu: Kichaka kinachowaka.
Chini: Kuvuka kwa Bahari ya Shamu



*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

PERIODICAL
Reading, PA

